**Jina la shughuli wezeshi**: Shughuli wezeshi ya kujenga uwezo wa kitaasisi katika kutekeleza Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni

Shughuli zilizotekelezwa

(i) Kukamilisha Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa marekebisho ya Kigali yanayohusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya hidrofluorokaboni (Hydrofluorocarbos – HFCs) ambazo zinasababisha ongezeko la joto duniani.

(ii) Kuandaliwa kwa Kanuni za Usimamizi wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la hewa ya Ozoni za Mwaka 2007 na imefanyiwa marekebisho ili kujumuisha kemikali zinazochangia mabadiliko ya Tabianchi na Kanuni ya sasa ni Kanuni za Usimamizi wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la hewa ya Ozoni za Mwaka 2022;

(iii) Mafunzo kwa Mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu zaidi ya **900** kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo bila kuathiri Tabaka la hewa ya Ozoni;

(iv) Kusambazwa kwa Vitambuzi **25** (refrigerant identifiers) vya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni katika vituo vya forodha vilivyo mipakani kwa ajili ya kusadia kutambua kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki Montreal wakati zinapoingizwa nchini;

(v) Kununua na kusimika mashine **25** za kunasa na kurejeleza gesi chakavu za Majokofu na Viyoyozi katika karakana **20** na Vituo vitano vya Kikanda katika vyuo vya VETA vya Mwanza, Chang'ombe - Dar es salaam, Kigoma, Mbeya na Mkokotoni-Zanzibar;

(vi) Mafunzo kwa maafisa wapatao **1000** kutoka Mamlaka ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA), Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni.

(vii) Kuviwezesha vyuo vya VETA, Chuo Kikuu cha Mbeya cha Sayansi na Teknolojia (MUST) na Chuo cha Kodi kupitia mitaala ya kufundishia kwa kozi zinazohusiana na uhudumiaji wa majokofu, viyoyozi na mitambo ya kupoozea pamoja na udhibiti wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Motreal; na

(viii) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa vyuo vya mafunzo ya elimu ya ufundi zaidi ya 100 kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo bila kuathiri Tabaka la Ozoni.

(ix) Mafunzo kwa wasimamizi wa sheria katika mipaka ya Namanga, Namanga, Horohoro, Holili, Uwanja wa Kimataifa wa Mwl Julius Nyerere, Bandari Kuu kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal